
# Kitu cha kusema kwenye kila sehemu ya Mchoro


Sehemu ya 1

“Mungu alimwumba kila mtu awe kwenye uhusiano pamoja naye na kuishi maisha yaliyobarikiwa. Hakupanga maisha yawe ni ya matatizo na mateso chungu zima.”




Sehemu ya 2


“Mwanadamu ametenganishwa na Mungu kwa sababu ya dhambi. Watu wa mwanzo walitenda dhambi, na tangu hapo kila mtu ametenda dhambi dhidi ya Mungu.”



Sehemu ya 3

"Mungu ni hakimu wa haki, na siku moja wenye dhambi watahukumiwa kwenda kwenye moto wa milele isipokuwa wawe wametafuta rehema za Mungu na kurejea kwenye uhusiano tena pamoja na Mungu."


[Chora mshale na andika neno "motoni."]




Sehemu ya 4

"Hakuna lolote tunaloweza kulifanya kwa ajili ya kuturejesha tena upya kwa Mungu au kupata rehema – siyo kwa matendo mema, siyo kwa kwenda kanisani, siyo taratibu za kimadhehebu, na wala siyo kutoa fedha...."


[Chora mshale kuonyesha kila kilichotajwa kwenye orodha.]



Sehemu ya 5

“Hali yetu ingekuwa mbaya sana kama Mungu hangefanya njia kwa ajili yetu ya kurejea kwake. Yesu, Mwana wa Mungu alikufa juu ya msalaba ili tuweze kusamehewa. Baada ya siku tatu, alifufuka kutoka kwa wafu.”


[Chora msalaba.]




Sehemu ya 6

“Lakini haitoshi tu kujua haya. Kila mtu binafsi atapaswa kufanya chaguo la kuokoka na kurejea tena kwa Mungu. Mtu ni lazima atubu, ikimaanisha kwamba ni kujutia kikamilifu kuhusu dhambi na kuwa tayari kwa hiari yake mwenyewe kuachana nazo. Mtu anayetubu anaweza kupata msamaha kwa kumsihi Mungu kwenye maombi.”

[Chora mshale kisha andika maneno “tubu” na “pokea.”]




Sehemu ya 7

"Ni wapi unapofikiri kwamba upo katika mchoro huu? Je, kumewahi kutokea kuwepo na muda maalumu katika maisha yako ambao ulitubu dhambi zako, ukapokea msamaha wa Mungu, na ukaanza kuishi kwa ajili ya Mungu; au bado umetengwa na Mungu kutokana na dhambi yako?”

[Subiri kupata jibu. Watu wengi watakiri kwamba bado wametengwa na Mungu.]

"Uko tayari kufuata hatua hii—Kutubu, kupokea msamaha, na kuanza kuishi kwa ajili ya Mungu? Nitapendezwa sana kuomba pamoja nanyi sasa hivi."

[Fanya maombi yanayokaribia kufanana na haya yafuatayo.]

"Bwana, ninajua mimi ni mwenye dhambi na ninayestahili adhabu ya milele. Ninajutia dhambi zangu na niko tayri kuachana nazo. Ninaomba unisamehe, siyo kwa sababu ninastahili, bali kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yangu. Asante kwa wokovu wako. Kuanzia sasa, nitaishi kwa ajili yako tu."